Ahadi za Serikali V

Zimekusanywa na HakiElimu

Januari-Julai 2009



Ahadi za Serikali V

Zimekusanywa na HakiElimu

Januari-Julai 2009

Shukrani

Utayarishaji wa chapisho hili la ***Ahadi za Serikali*** usingeweza kukamilika bila michango kutoka kwa watu mbalimbali. Shukrani za kwanza ni kwa Fredrick Msigallah kwa kukusanya ahadi na maagizo ya ya viongozi wa serikali kutoka katika magazeti mbalimbali na kuandaa muhutasari wa chapisho hili. Pia tunapenda kutambua mchango kutoka kwa Mkurugenzi Mtendaji, Elizabeth Missokia, Samuel Saigurani na Gervas Zombwe kwa kuhariri na kusimamia utayarishaji na uchapishaji wa chapisho hili. Kipekee pia tunawashukuru wafanyakazi wote wa Idara ya Uchambuzi wa Sera na Utetezi ya HakiElimu kwa kuchangia mawazo yao yaliyosaidia kufanikisha kazi hii. Picha ya jalada ni jengo la darasa la wanafunzi wa darasa la sita iliyopigwa huko Simanjiro Julai 2008. Taarifa zote zimetolewa katika magazeti ya Tanzania ambayo mchango wake katika kutoa taarifa huru ni muhimu sana kwetu sote.

©HakiElimu, 2009

HakiElimu

S. L. P 79401,

Dar es Salaam,

Tanzania.

Simu: 255 22 2151852/3

Nukushi: 255 22 2152449

Barua pepe: info@hakielimu.org

Tovuti: www.hakielimu.org

ISBN 9987-423-89-2

Utangulizi

Huu ni mwaka wa nne wa serikali ya awamu ya nne ambayo kauli mbiu yake imekuwa ni ***"Maisha bora kwa kila Mtanzania".*** Ahadi hii ilitolewa na serikali kwa Watanzania wakati ilipoingia madarakani mwaka 2005. Kama ilivyoainishwa katika Dira ya Maendeleo ya Tanzania, 2025 na MKUKUTA, moja ya malengo ya serikali ya awamu ya nne ni kuboresha na kuimarisha utawala bora ili kuleta maendeleo endelevu. Utawala bora una misingi yake, baadhi ya misingi hiyo ni pamoja na utawala wa sheria, uwajibikaji, uwazi, kuheshimu haki za binadamu, demokrasia, kupiga vita rushwa na ufisadi na ushirikishwaji wa wananchi katika masuala yanayowahusu.

Katika jamii yoyote ile ya kidemokrasia, matendo na kauli za viongozi wa serikali vinapaswa kufuatiliwa na wananchi ili kuhakikisha kuwa viongozi au serikali husika inawajibika kikamilifu kwa wananchi ambao ndiyo walioiweka madarakani. Kupitia vyombo vya habari, mikutano na ilani za vyama, serikali imekuwa ikitoa ahadi mbalimbali kwa wananchi na maagizo kwa watendaji wake yenye lengo la kuboresha utendaji wa serikali katika kuwahudumia wananchi. Mwananchi unapaswa kujiuliza, je serikali inatimiza ahadi zake?, kama haitimizi, ni kwa nini? Na kama inatimiza, ni kwa kiasi gani?. Katika ufuatiliaji huu, sifa zinapaswa kutolewa pale inapostahili na maelezo zaidi kudaiwa pale ambapo serikali inashindwa kutekeleza ahadi zake ipasavyo.

Wananchi wanapaswa kuwa na taarifa za kutosha kuhusu ahadi za serikali yao ili waweze kufutilia kikamilifu utekelezaji wake. Hata hivyo wananchi wengi hawajui kuwa hii ni haki yao ya msingi na hawana taarifa juu ya ahadi zinazotolewa na serikali, na hivyo kufanya kazi yao ya kufuatilia kuwa ngumu.

Hali hii imesababisha ahadi nyingi kutotekelezwa. Kuwaelimisha wananchi juu ya haki na wajibu wao pamoja na kuwapa taarifa mbalimbali kuhusu maendeleo yao kutawasaidia sana kufuatilia utendaji wa serikali yao na hivyo kuifanya iwajibike ipasavyo .

Kama sehemu ya kazi zake za uchechemzi, HakiElimu imekuwa ikifuatilia ahadi na maagizo mbalimbali yanayotolewa na viongozi wa serikali kupitia vyombo vya habari hususan magazeti. Ahadi na maagizo hayo hukusanywa pamoja na kisha kutayarisha kijitabu cha ***"Ahadi za Serikali"***. Kijitabu hiki huonesha kiongozi aliyetoa ahadi, ahadi au agizo alilotoa na chombo cha habari ambacho ahadi au agizo hilo liliripotiwa.

Lengo hasa la kutayarisha kijitabu hiki ni kuwataarifu wananchi kile ambacho serikali yao imewaahidi pamoja na kuwajengea uwezo wa wao kuiwajibisha serikali. Si hivyo tu, pia kijitabu hiki kinaweza kutumika kama zana ya kufanyia tathmini utendaji wa serikali na hivyo kuweza kupima uwezo wa serikali katika utekelezaji wa majukumu yake ikiwa ni pamoja na ahadi inazotoa kwa wananchi wake.

Mkusanyiko huu wa ahadi unajumuisha ahadi na maagizo yaliyotolewa na viongozi wa serikali katika ngazi mbali mbali katika kipindi cha Januari hadi Juni 2009. Ahadi na maagizo yaliyomo katika kijitabu hiki ni pamoja yale yanayohusu elimu, ustawi wa jamii, utawala bora, kilimo, afya, miundombinu, nishati, maji, usalama barabarani, demokrasia na mazingira. Taarifa zote zimechukuliwa katika magazeti, na yote yameoneshwa kwa ajili ya rejea.

Kama ilivyokuwa katika machapisho yaliyopita, chapisho hili halikusudii kuwa na ufafanuzi wa kina sana bali linatoa maelezo ya jumla kuhusu ahadi za serikali. Kwa wale watakaohitaji kupata maelezo ya kina wanashauriwa kuangalia tovuti ya serikali kupitia anuani hii: www.tanzania.go.tz au kufanya mawasiliano na wizara husika. Chapisho hili linaonesha ahadi zilizotolewa na serikali, lakini halitoi taarifa ya utekelezaji wake. Jukumu hilo ni lako wewe msomaji hivyo timiza wajibu wako kwa serikali ili serikali ikutumikie wewe sawa sawa na ilivyokuahidi.

MAAGIZO NA AHADI ZILIZOTOLEWA NA RAIS NA VIONGOZI WENGINE WA NGAZI ZA JUU SERIKALINI (KUANZIA JANUARI-JUNI 2009)

KIONGOZI	AHADI/MAAGIZO	MWANDISHI/GAZETI
Mkuu wa Wilaya, Abihudi Saideya, Meatu-Shinyanga.	Utawala Bora (Usimamizi wa fedha za umma): Serikali imeuagiza uongozi wa Halmashsuri ya Wilaya ya Meatu kusimamia vizuri fedha inazotoa kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za maendeleo ya wananchi. Agizo hilo lilitolewa na Mkuu wa Wilaya ya Meatu, Abihudi Saideya katika kikao cha ushauri cha wilaya baada ya kubainika kuwa fedha zilizotolewa na serikali bado hazijatumika vizuri kuboresha elimu na kuwapunguzia wanachi mzigo wa kuchangia sekta hiyo	Stephen Wang'anyi, Nipashe, 5 Januari 2009, uk. 10
Mkuu wa Mkoa, Dr Yohana Balele, Shinyanga.	Elimu (Chakula kwa wanafunzi): Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Dr Yohana Balele amewaagiza wakuu wa wilaya na wakurugenzi watenedaji wa halmashauri na manispaa kubuni mbinu za kuwapatia chakula cha mchana shuleni wanafunzi wa shule za msingi ili kuinua kiwango cha taaluma. Agizo hilo lilitolewa katika mkutano wa wadau wa elimu wa kutathmini matokeo ya mtihani wa taifa wa darasa la saba uliofanyika mwishoni mwa mwaka jana.	Stephen Wang'anyi, Nipashe, 6 Januari 2009, uk. 15
Waziri Mkuu, Mizengo Pinda, Mpanda, 5 Januari 2009.	Utawala Bora: Waziri Mkuu Mizengo Pinda amewaagiza maafisa watendaji wa vijiji na kata nchini kuacha kukusanya michango ya vitu na fedha toka kwa wakulima kwa njia za manyanyaso hususan wakati wa msimu wa kilimo. Alisema vitendo hivyo vinarudisha nyuma juhudi za serikiali za kuboresha uzalishaji katika sekta ya kilimo. Waziri Mkuu aliyaesma hayo wakati akihutubia vijana kutoka sehemu mbali mbali za wilaya ya Mpanda.	Mwandishi, Daily News, 6 Januari 2009, uk. 2.
Naibu Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, Dr. James Wanyancha, Serengeti.	Utawala bora (uwazi katika mapato na matumizi ya fedha za umma): Mbunge wa Serengeti, Dr. James Wanyancha amewapa muda wa wiki mbili maofisa watendaji wa vijiji na kata katika wilaya hiyo kutoa ripoti ya taarifa ya mapato na matumizi kwa wananchi. Aliwataka viongozi hao kutoa ripoti ya michango ya wananchi iliyotolewa awali kabla ya kuwaomba wananchi kutoa michango mipya ya shughuli za maendeleo katika maeneo yao	Anthony Mayunga, THE CITIZEN, 9 Januari 2009, uk 5.
Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, John Chiligati, Moshi.	Makazi: Serikali imeliagiza Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) kuelekeza nguvu zake katika kujenga nyumba za makazi na kuziuza kwa wananchi badala ya kukusanya kodi za pango kama ilivyo sasa. Agizo hilo lilitolewa na Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makazi, John Chiligati wakati alipokuwa akikagua miradi mbalimbali ya NHC tawi la Moshi.	Grace Macha, Tanzania DAIMA, 12 Januari 2009, uk. 5
Rais Jakaya Kikwete, Dar es Salaam, 13 Januari 2009.	Makazi bora: Serikali imeahidi kuboresha mazingira ya kazi kwa askari polisi nchini kwa kuongeza mishahara yao pamoja na kuwapa makazi bora. Ahadi hiyo ilitolewa na Rais Jakaya Mrisho Kikwete wakati akizindua rasmi nyumba 283 zilizojengwa kwaajili ya makazi ya polisi zilizopo katika eneo la Kurasini.	Consesa John, THE CITIZEN, 14 Januari 2009, uk. 4

KIONGOZI	AHADI/MAAGIZO	MWANDISHI/GAZETI
Rais Jakaya Kikwete, Dar es Salaam, 15 Januari 2009.	**Usafirishaji (Bandari):** Rais Jakaya Kikwete ameiagiza Mamlaka ya Bandari kuyapiga mnada makontena yote yatakayokuwa yamekaa bandarini siku 21 baada ya kuwasili bila wamiliki wake kuyachukua. Rais alitoa agizo hilo ili kupunguza mlundikano wa makontena katika bandari ya Dar es Salaam. Rais alitoa agizo hilo katika mkutano wake na watendaji wakuu wa wizara ya Miundombinu na Usafirishaji. Sambamaba na hilo, aliwataka wafanya kazi wa Mamlaka ya Kodi ya Mapato (TRA) kuboresha utendaji wao wa kazi ikiwa ni pamoja na kuongeza muda wa kufanya kazi hadi kufikia masaa 24.	Reporter, THE CITIZEN, 16 Januari 2009, uk 1.
Rais Jakaya Kikwete Dar es Salaam.	**Usafirishaji:** Rais Jakaya Kikwete ameiagiza menejimenti ya Kampuni ya Ndege nchini (ATCL) kuhakikisha kuwa huduma zake za ndege zinarejeshwa haraka iwezekanavyo. Rais alitoa agizo hilo wakati alipokutana na uongozi wa Wizara ya Miundombinu, wakiwemo wakuu wa ATCL katika mikutano yake na wizara mbalimbali kutathimini utendaji wa serikali yake na mashirika yaliyoko chini ya wizara hizo kwa kipindi cha miaka mitatu ya uongozi wake.	Mwandishi Maalum, Nipashe, 18 Januari 2009, uk. 1
Waziri wa Maji na Umwagiliaji, Prof. Mark Mwandosya, Mugumu-Serengeti.	**Maji:** Serikali imeahidi kumaliza tatizo sugu la upungufu wa maji katika mji wa Mugumu, wilayani Serengeti kwa kuweka mfumo mpya wa kusambaza maji. Ahadi hiyo ilitolewa na Waziri wa Maji na Umwagiliaji, Prof. Mark Mwandosya.	Anthony Mayunga, THE CITEZEN, 19 Januari 2009, uk 4
Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, Mwantumu Mahiza, Handeni.	**Elimu:** Wakuu wa wilaya mkoani Tanga wameagizwa kuhakikisha kuwa wanafunzi wote (5,016) waliokosa nafasi shule za sekondari wanajiunga na kidato cha kwanza mwaka huu. Agizo hilo lilitolewa na Naibu waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, Mwantumu Mahiza wakati akifanya majumuisho ya ziara yake katika baadhi ya wilaya za mkoa wa Tanga. Mahiza aliwataka kuharakisha ujenzi wa madarasa ili kufanikisha zoezi hilo la kuwapeleka wanafunzi wote sekondari.	Sonyo Mwenkale, Nipashe, 20 Januari 2009, uk 15
Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa), Celina Kombani Dar es Salaam.	**Elimu (Malimbikizo ya walimu):** Serikali imetoa kauli kwamba iko katika hatua za mwisho za kuhakiki malimbikizo ya mishahara ya walimu wa shule za msingi na sekondari. Kauli hiyo ilitolewa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa), Celina Kombani.	Reporter, Daily News, 20 Januari 2009, uk. 3.
Waziri Mkuu, Mizengo Pinda, Chato, 19 Januari 2009.	**Vita dhidi ya mauaji ya albino:** Waziri Mkuu, Mizengo Pinda ameviagiza vyombo vya kisheria kutoa adhabu kali kwa wahalifu wa mauaji ya albino. Agizo hilo lilitolewa kama sehemu ya mkakati wa kupambana na uhalifu huo. Waziri Mkuu alitoa agizo hilo wakati wa uzinduzi wa tawi la banki ya NMB Chato pamoja na nyumba za Shirika la Nyumba la Taifa (NHC)	Grace Chilongola, Nipashe, 21 Januari 2009, uk. 5
Rais Jakaya Kikwete Zanzibar 24 January.	**Usalama barabarani:** Rais Jakata Kikwete ameliagiza jeshi la polisi kuhakikisha sheria za usalama barabarani zinatekelezwa kikamilifu ili kupunguza ajali za barabarani. Rais alitoa agizo hilo wakati akihutubia wakazi wa Bumbwini katika ziara yake ya kutembelea mkoa wa Zanzibar Kaskazini.	Tuma Abdallah, Sundaynews, 25 Januari 2009, uk 1

KIONGOZI	AHADI/MAAGIZO	MWANDISHI/GAZETI
Waziri wa Fedha na Uchumi, Mustapha Mkulo Morogoro.	Elimu (chakula shule za sekondari): Serikali imeahidi kutatua tatizo la ukosefu wa chakula kwa shule zake za sekondari katika kipindi cha mwaka huu. Ahadi hiyo ilitolewa na Waziri wa Fedha na Uchumi, Mustapha Mkulo wakati akizungumza katika mahafali ya kidato cha Sita ya Shule ya Sekondari ya Dakawa iliyopo wilayani Mvomero Mkoa wa Morogoro.	Fitina Haule, Nipashe, 29 Januari 2009, uk. 15
Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, John Chiligati, Dar es Salaam 29 Januari 2009.	Makazi: Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mh. John Chiligati amesema kuwa watu wanaoishi katika maeneo ya Kivukoni na Mji Mwema, Kigamboni hawatahamishwa kutoka katika maeneo hayo ili kupisha uendelezaji wa eneo hilo kuwa mji mpya na wa kisasa. Mh. Chiligati alisema wale watakao lazimika kuhama, watafidiwa na kupewa maeneo mapya katika eneo hilo hilo la Kigamboni au watakuwa sehemu ya mradi utakaoanzishwa. Waziri aliyasema hayo bungeni wakati akijibu swali la Mh. Ania Chaurembo, Mbunge wa Viti Maalum -CUF, aliyetaka kujua tamko la serikali juu ya kuwahamisha wakazi hao wa Kigamboni ili kupisha mradi huo.	Mwandishi, Daily News, 30 Januari 2009, uk 2.
Mbunge wa Singida Kaskazini, Lazaro Nyalandu, Singida.	Ufadhili wa miradi ya maendeleo: Mbunge wa Singida kaskazini, Lazaro Nyalandu ameahidi kufadhili miradi mbali ya maendeleo yenye thamani ya Sh 1.1 billion katika jimbo lake la uchaguzi. Nyalandu alisema atatoa ufadhili huo katika kipindi cha miezi sita ijayo. Alitoa ahadi hiyo alipokuwa akiwahutubia wananchi wa kata ya Ilongore. Alisema ufadhili huo ni sehemu ya juhudi zake za kuchangia maendeleo ya wananchi.	Gasper Andrew, THE CITIZEN, 9 Febrauri 2009, uk. 6
Waziri Mkuu, Mh. Mizengo Pinda, Moshi, 7 Februari 2009.	Mazingira (Usimamizi wa sheria): Waziri Mkuu, Mzengo Pinda ameagiza halmashauri zote nchini na watendaji wake kusimamia vema sheria za mazingira ikiwemo utunzaji wa vyanzo vya maji ambavyo kwa asilimia kubwa vinaonekana kupotea. Waziri Mkuu alitoa agizo hilo mkoani Kilimanjaro wakati akikagua miradi mbalimbali ya maendeleo ukiwemo mradi wa kilimo cha umwagiliaji wa Lower Moshi ulioko wilaya ya Moshi vijijini	Salome Kitomary na Charles Lyimo, Nipashe 18 Februari 2009 Uk 2
Rais Jakaya Kikwete, Dar es Salaam, 18 Februari 2009.	Elimu (Kuvuja kwa mitihani): Rais Jakaya Kikwete amemwagiza waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi Prof. Jumamne Maghembe kulisafisha Baraza la Mitihani Tanzania kutokana na kukithiri kwa vitendo vya wizi wa mitihani. Rais alitoa agizo hilo wakati alipokutana na viongozi wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi pamoja na taasisi zilizoko chini ya wizara hiyo. Aliyasema hayo wakati akiwa katika awamu yake ya pili ya kukutana na wizara mabli mbali ili kuangalia utendaji wa kazi zake. Pia aliagiza kuangaliwa upya kwa mfumo mzima wa usimamizi wa mitihani kwa lengo la kuimarisha zaidi usalama wa nyaraka zote za mitihani.	Mwandishi THE CITEZEN, 20 Februari 2009, uk 2
Waziri wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Celina Kombani, Morogoro, 19 Februari 2009.	Demokrasia (Uchaguzi wa serikali za mitaa): Waziri wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Celina Kombani ameahidi kuwa serikali itahakikisha kuwa Uchaguzi wa Serikali za Mitaa nchini utakaofanyika Oktoba mwaka huu utakuwa wa amani na utulivu. Waziri alitoa ahadi hiyo katika mkutano wa viongozi wa vyama vya siasa, wakurugenzi wa halmashauri na watendaji wakuu wa asasi zisizo za kiserikali kujadili maandalizi ya uchaguzi huo. *Nukuu: "Tanzania ni taifa moja tangu lilipopata uhuru takribani miaka 47 iliyopita, imekuwa na tabia ya kujadiliana na kukubaliana bila kugombana wala kusuguana katika chaguzi hivyo ni vyema kuendelea kushindana katika kupata uongozi bila vurugu."*	Ashton Balaigwa Nipashe, 21 Februari 2009, uk 26.

KIONGOZI	AHADI/MAAGIZO	MWANDISHI/GAZETI
Rais Jakaya Kikwete, Dar es Salaaam, 20 Februari 2009.	**Utafiti:** Rais Jakaya Kikwete ametangaza kuongezwa kwa fedha kwa ajili ya utafiti kutoka asilimia 0.03 ya sasa hadi asilimia 1 ya pato la ndani la taifa (GDP) katika mwaka wa fedha ujao. Rais alitoa ahadi hiyo katika mkutano wake na maafisa wa Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko uliofanyika jijini Dar es Salaam.	Reporter, THE CITIZEN, 21 Februari 2009, uk. 3
Mkuu wa Wilaya ya Kinondoni, Fabian Massawe.	**Mapambano dhidi ya mauaji ya albino (Uganga wa kienyeji):** Serikali ya wilaya ya Kinondoni mkoani Dar es Salaam imewaagiza watendaji wa kata zote 27 na madiwani wake kusimamia zoezi la ung'oaji wa mabango yote ya waganga wa kienyeji. Agizo hilo lilitolewa na Mkuu wa Wilaya ya Kinondoni, Fabian Massawe ikiwa ni sehemu ya mapambano dhidi ya mauaji ya albino nchini.	Abdul Mitumba, Nipashe, 24 Febrauari 2009, uk. 2
Rais Jakaya Kikwete, Dar es Salaam, 01 Machi 2009.	**Elimu (Uhamisho wa watumishi wa umma):** Rais Jakaya Kikwete amesema kuanzia sasa maafisa watakaojihusisha na uhamishaji usio wa lazima wa watumishi wa serikali, watawajibika kulipa gharama za uhamisho huo wao wenyewe. Agizo hilo limetolewa ili kukabiliana na tatizo la malimbikizo ya madeni ya watumishi wa umma yanayotokana na kupandishwa vyeo, uhamisho na malipo ya likizo ambayo kwa mujibu wa Rais, yametokana na utendaji usioridhisha wa maafisa wandamizi wa idara zinazohusika na malipo hayo. Rais alitoa tamko hilo katika utaratibu wake wa kawaida wa kulihutubia taifa kila mwezi.	Reporter, Daily News, 2 Machi 2009, uk. 1
Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, Gaudensia Kabaka, Bunda.	**Elimu (Uhaba wa walimu shule za sekondari):** Serikali imeahidi kuwa muda si mrefu, shule zote za sekondari zilizojengwa na wananchi, zitakuwa na walimu wa kutosha. Kauli hiyo imetolewa na Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, Gaudensia Kabaka wakati akiwahutubia wanawake wa Jumuiya ya Wanawake wa CCM na wanachuo wa Chuo cha Ualimu Bunda. Alisema tatizo la upungufu wa walimu linalozikabili shule nyingi hivi sasa ni la muda mfupi, kati ya mwaka mmoja au miwili na baada ya hapo tatizo hilo litakuwa limemalizika. Sambamba na hilo Naibu Waziri amesema pia serikali itahakikisha kuwa shule zote za sekondari zinakuwa na maabara.	Ahmed makongo, KULIKONI, 3 Machi 2009, uk. 4
Makamu wa Rais, Dr. Ali Mohammed Shein, Mafia, 2 Machi 2009.	**Miundombinu (Usafirishaji):** Serikali imeahidi kupeleka maendeleo katika kisiwa cha Mafya mkoani Pwani ikiwa ni pamoja na kuboresha miundombinu. Miundombinu itakayoboreshwa ni pamoja na ujenzi wa uwanja wa ndege ambao utelezaji wake tayari umeanza na Bandari ya Kilindoni. Makamu wa Rais alitoa ahadi hiyo wakati akihutubia mkutano wa hadhara uliofanyika Mkunguni kisiwani hapo.	Mwandishi, Nipashe, 3 Machi 2009, uk. 2
Rais Jakaya Kikwete, Dar es Salaam, 3 March 2009.	**Maliasili (madini):** Rais Jakaya Kikwete ameagiza sekta ya madini isimamiwe kikamilifu kwa kuhakikisha wenye leseni za kutafuta na kuchimba madini wanazitumia kwa masharti yaliyoombewa, kinyume na hivyo, wanyang'anywe leseni hizo. Rais alitoa agizo hilo katika mkutano wake wa tathmini ya utendaji wa serikali yake na Uongozi wa Wizara ya Nishati na Madini na taasisi zake. Sambamba na hilo alimwagiza kamishna wa madini nchini kuchukua hatua za haraka kukomesha uchimbaji wa kokoto katika maeneo yasiyoruhusiwa.	Mwandishi, Kulikoni, 5 Machi 2009, uk. 5
Waziri wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Celina Kombani, Ulanga, 12 Machi 2009.	**Elimu:** Waziri wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Celina Kombani amewaagiza wakurugenzi wa Halmashauri nchini kuandaa utaratibu wa kuwapatia mafunzo ya mara kwa mara walimu wa shule za msingi ili kuinua kiwango chao cha elimu. Waziri alitoa agizo hilo wakati akifungua mafunzo ya kuboresha masomo ya Hisabati na Kiingereza kwa walimu wa wilayani Ulanga.	Ashton Balaigwa, Nipashe, 14 Machi 2009, uk.25.

KIONGOZI	AHADI/MAAGIZO	MWANDISHI/GAZETI
Waziri Mkuu, Mizengo Pinda, Dar es Salaam, 13 Machi 2009.	Malipo ya fidia: Waziri Mkuu, Mizengo Pinda ameliagiza Shirika la Maji Safi na Maji Taka Dar es Salaam (DAWASCO) kupitia upya malipo ya fidia yaliyotolewa kwa wananchi wa eneo la Kurasini Shimo la Udongo jijini Dar es Salaam kwa kuwa malipo waliyolipwa awali yalikuwa ni kidogao. Waziri Mkuu aliyasema hayo alipokuwa katika ziara yake ya siku nne ya kutembelea jiji la Dar es Salaam ambapo alitembelea bwawa la maji taka lililopo eneo la Kurasini Shimo la Udongo.	Abdulwakil Saiboko, Daily News, 14 Machi 2009, uk 3
Waziri Mkuu, Mizengo Pinda, Dar es Salaam, 15 Machi 2009.	Utawala bora (Makusanyo ya ushuru): Waziri Mkuu Mizengo Pinda ameiagiza Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kufanya uchunguzi wa mapato na matumizi ya makusanyo ya Kituo cha Mabasi cha Ubungo na Soko la Kariakoo ili kuboresha mapato ya Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam. Pinda alitoa agizo hilo wakati akiwahutubia viongozi mbalimbali wa mkoa wa Dar es Salaam wakati wa majumuisho ya ziara yake ya siku nne ya mkoa huo. Waziri Mkuu alitoa agizo hilo baada ya kutoridhishwa na hali ya ukusanyaji wa mapato katika maeneo hayo mawili ambayo kwa mujibu wake yangeweza kulipatia jiji mapato makubwa.	Mwandishi, Kulikoni, 16 Machi 2009, uk. 2
Meneja wa Tanroads Mkoa wa Rukwa, Mr. Joseph Nyamhanga, Sumbawanga.	Miundombinu (Ukarabati wa barabara): Serikali imeahidi kuendelea na ukarabati, utunzaji na usimamizi wa barabara zinazokadiriwa kuwa na urefu wa zaidi ya kilometa 363.78 katika mkoa wa Rukwa ikiwa ni juhudi zake za kuhakikisha kuwa barabara hizo zinapitika katika kipindi chote cha mwaka. Ahadi hiyo ilitolewa na Meneja wa Tanroads Mkoa wa Rukwa Bwana Joseph Nyamhanga.	Peti Siyame, Daily news, 18 Machi 2009, uk. 2.
Katibu Mkuu, Wizara ya Fedha na Uchumi, Ramadhani Khijjah, 17 Machi 2009.	Kilimo (Pembejeo za kilimo): Serikali imepanga kutoa ruzuku ya pembejeo za kilimo kwa wakulima wapatao milioni tatu ikiwa ni zaidi ya wakulima 700,000 ambao kwa sasa wanapata huduma hiyo. Kauli hiyo ilitolewa na Katibu Mkuu, Wizara ya Fedha na Uchumi, Ramadhani Khijjah alipokuwa akihutubia mkutano wa wawekezaji wa ndani. Khijjah alisema hatua hiyo ni sehemu ya utekeleza wa Mpango kambambe wa Maendeleo ya Sekta ya Kilimo nchini Tanzania na kwamba Rais ameagiza utekelezaji wa agizo hili uanze katika msimu ujao wa kilimo.	Pius Rugonzibwa, Daily News, 18 Machi 2009, uk. 3
Waziri Mkuu, Mizengo Pinda, Dar es Salaam.	Kodi kwenye mishahara: Wizara ya Fedha na Uchumi imetakiwa kuangalia upya viwango vya kodi na kiwango cha kuanza kutoza kodi ya mapato sambamba na kubaini vyanzo vipya ili kufidia pengo litakalotokana na marekebisho hayo. Agizo hilo lilitolewa na Waziri Mkuu Mizengo Pinda wakati alipokutana na viongozi wa vyama vya wafanyakazi ofisini kwake jijini Dar es Salaam.	Nipashe, 21 Machi 2009, uk.1
Waziri Mkuu, Mizengo Pinda, Kilosa, Morogoro.	Utawala bora (matumizi ya fedha za umma): Waziri Mkuu Mizengo Pinda amezitaka halmashauri za wilaya nchini kuacha kutenga bajeti kubwa ikiwemo ya ununuzi wa mashangingi ya kifahari kwaajili ya watendaji wao. Waziri Mkuu aliyasema hayo wakati akizungumza na watendaji wa wilaya ya Kilosa mkoani Morogoro kwenye majumuisho ya ziara yake wilayani humo. Sambamba na hilo, aliutaka uongozi wa serikali na halmashauri ya wilaya hiyo kutumia sh milioni 400 zilizokusanywa kama faini katika operation ya wafugaji, kuboresha mazingira ya wafugaji hao.	Joseph Malembeka, Tanzania DAIMA, 2 April 2009, uk. 3

KIONGOZI	AHADI/MAAGIZO	MWANDISHI/GAZETI
Naibu Waziri katika Ofisi ya Waziri Mkuu-TAMISEMI, Aggrey Mwanri, Dodoma, 24 Aprili 2009.	Mgawanyo wa fedha (kwaajili ya wanawake na vijana): Serikali imeziagiza halmashauri za wilaya/miji/manispaa/jiji kote nchini kutenga asilimia 10 ya mapato yao kwaajili ya Mfuko wa Wilaya wa Maendeleo ya Wanawake na Vijana. Agizo hilo lilitolewa na Naibu Waziri katika Ofisi ya Waziri Mkuu-TAMISEMI, Aggrey Mwanri bungeni mjini Dodoma wakati akijibu swali la Laus Mhina (Korogwe vijijini) ambaye alitaka kujua hatua zianazochukukuliwa dhidi ya halmashauri ambazo hazitengi fedha kwaajili ya mfuko huo. Naibu Waziri alizitaka halmashauri zote kutekeleza agizo hilo mara moja na kutoa taarifa ya utekelezaji katika ofisi yake kila baada ya miezi mitatu.	Daily News, 25 Aprili 2009, uk. 2
Naibu Waziri wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, Dk. Lucy Nkya, Dodoma.	Uchumi (Ujasiria mali): Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na watoto imeahidi kujenga kituo cha kitaifa cha biashara jijini Dar es Salaam. Kituo hicho kitatumika kutoa mafunzo ya ujasiria mali ili kuboresha biashara na bidhaa za wajasiria-mali. Ahadi hiyo ilitolewa na Naibu Waziri wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, Dk. Lucy Nkya bungeni Dodoma wakati akijibu swali la Mbunge wa Viti Maalum kwa tiketi ya Chadema, Anna Komu, aliyehoji ni kwa nini serikali isiwawezeshe wanawake kuboresha bidhaa zao wanazotengeneza ili ziwasaidie kuinua kipato chao.	Kulikoni, 28 April 2009, uk. 5
Naibu Waziri wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, Gaudensia Kabaka, Dodoma, 28 Aprili 2009.	Elimu ya ufundi: Serikali imesema imepata fedha za kujenga vyuo vitatu vya ufundi katika mikoa mitatu isiyokuwa na vyuo hivyo ambayo ni Pwani, Manyara na Lindi. Kauli hiyo ilitolewa na Naibu Waziri wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, Gaudensia Kabaka mjini Dodoma wakati akijibu swali la Mbunge wa Viti maalum, Fatma Abdallah Mikidadi (CCM), aliyetaka kujua idadi ya mikoa isiyokuwa na vyuo hivyo nchini na utekelezaji wa ahadi ya serikali ya kujenga chuo cha VETA mkoani Lindi. Gaudensia alisema fedha hizo zimepatikana kwa ushirikiano wa serikali ya Tanzania na Serikali ya Jamhuri ya Watu wa Korea.	Nipashe, 29 April 2009, uk. 11
Naibu Waziri wa Miundombinu, Hezekiah Chibulunje, Dodoma, 28 Aprili 2009.	Miundombinu (daraja): Serikali imeahidi kutoa kipaumbele kwa bajeti ya 2009/10 ili kumalizia ujenzi wa daraja la Mto Lukamba lililoko katika jimbo la Nanyumbu. Ahadi hiyo ilitolewa na Naibu Waziri wa Miundombinu, Hezekiah Chibulunje wakati akijibu swali la Mbunge Dunstan Mkapa wa jimbo la Nanyumbu (CCM) aliyetaka kufahamu ujenzi wa daraja hilo utakamilika lini. Chibulunje alisema mchakato wa awali wa ujenzi wa daraja hilo tayari umekwisha kukamilika.	Kulikoni, 29 April 2009, uk. 5.
Waziri wa Kilimo na Ushirika, Stephen Wasira, Dodoma, 28 Aprili 2009.	Chakula: Serikali imeahidi kutoa msaada wa chakula katika maeneo yote yaliyoathirika na njaa ili kuwanusuru wananchi wanaokabiliwa na janga hilo. Sambamba na hilo serikali pia imeahidi kufanya tathmini ya hali ya chakula katika maeneo yenye hali mbaya zaidi. Ahadi hiyo ilitolewa na Waziri wa Kilimo na Ushirika, Stephen Wasira wakati akijibu swali la Mbunge wa jimbo la Mtera, John Malecela (CCM), aliyetaka kujua ni kwa nini wizara hiyo imetoa kipaumbele kwa wilaya ya Mpwapwa katika kupewa msaada wa chakula wakati hali hiyo imeukumba mkoa wote wa Dodoma.	Kulikoni, 29 April 2009, uk. 5.
Waziri Mkuu, Mizengo Pinda, Dodoma.	Utawala bora (Matumizi ya fedha za umma): Wizara, mikoa, halmashauri za wilaya na taasisi zote za serikali zimeagizwa kujadili kwa kina ripoti ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa serikali (CAG) na kutoa taarifa kwa Waziri Mkuu juu ya hatua zilizochukuliwa kukabiliana na udhaifu ulioripotiwa katika ripoti hiyo kabla ya mwisho wa Mkutano wa 16 wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania . Agizo hilo lilitolewa na waziri Mkuu, Mh. Mizengo Pinda wakati akifunga rasmi mkutano wa 15 wa Bunge mjini Dodoma.	Orton Kiishweko, The CITIZEN, 1 Mei 2009, uk. 3.

KIONGOZI	AHADI/MAAGIZO	MWANDISHI/GAZETI
Rais Jakaya Mrisho Kikwete, Arusha.	Miundombinu (Barabara): Serikali imetangaza mradi mkubwa wa kuboresha barabara katika maeneo ya kati ya nchi na hivyo kuyafungulia milango ya kibiashara. Maboresho hayo yatahusisha upanuaji wa barabara za Minjingu-Babati-Singida na Babati-Iringa-Dodoma. Kauli hiyo ilitolewa na Mh. Kikwete wakati wa uzinduzi wa ujenzi wa barabara ya Arusha-Athi River.	Zephania Ubwani, The CITIZEN, 1 Mei 2009, uk. 6.
Rais Jakaya Mrisho Kikwete, Arusha.	Usalama wa chakula: Rais Jakaya Mrisho Kikwete amewahakikishia Watanzania kuwa hakuna atakayekufa kwa njaa katika kipindi hiki ambacho maeneo mengi nchini yanakabiliwa na upungufu mkubwa wa chakula kutokana na uhaba wa mvua. Rais alitoa kauli hiyo wakati akihutubia wakazi wa Arusha wakati wa uzinduzi wa barabara ya Namanga hadi Arusha.	Cynthia Mwilolezi, Nipashe, 1 Mei 2009, uk. 9.
Naibu Waziri wa Miundombinu, Hezekiah Chibulunje, Dodoma.	Miundombinu: Serikali kupitia Mamlaka ya Usafirishaji wa Nchi Kavu na Majini (SUMATRA), imeiagiza Kampuni ya Reli Tanzania (TRL) kuhakikisha kuwa inaweka alama zote za tahadhari kwenye njia panda za barabara na njia za reli. Agizo hilo lilitolewa bungeni na Naibu Waziri wa Miundombinu, Hezekiah Chibulunje. Pia kampuni hiyo imeagizwa kuhakiksha kwamba madereva wa treni wanapiga honi wanapokaribia njia panda ili kuongeza tahadhari wakati wa kupita katika njia panda ambazo hazina vizuizi au walinzi.	Mary Edward, Nipashe, 2 Mei 2009, uk. 9
Waziri Mkuu, Mizengo Pinda, Mbinga, 4 Mei 2009.	Utawala bora (Matumizi ya fedha): Waziri Mkuu, Mizengo Pinda, amemwagiza Mkuu wa wilaya ya Mbinga, Kanali (mstaafu) Edmund Mjengwa kufuatilia na kuhakiki matumizi ya sh. Bilioni 1.5 za ujenzi wa mabanio na mifereji ya umwagiliaji katika miradi 19 ambayo matokeo yake yamekuwa hafifu. Waziri Mkuu alitoa agizo hilo baada ya kupokea taarifa ya kilimo ya wilaya hiyo na kutoridhishwa na maelezo yaliyotolewa katika taarifa hiyo kuhusu utekelezaji wa miradi hiyo.	Nipashe, 5 Mei 2009, uk. 5.
Makamu wa Rais, Dk. Mohamed Shein, Mwanza, 4 Mei 2009.	Utawala bora (Usalama wa raia): Serikali inatarajia kuandaa mswada wa sheria utakaowahakikishia hifadhi na usalama zaidi wa watu wenye ulemavu nchini wakiwemo maalbino. Mpango huo wa serikali ulitangazwa na Makamu wa Rais, Dk. Mohamed Shein wakati akihutubia Maazimisho ya Nne ya Siku ya Maalbino nchini yaliyofanyika katika Uwanja wa CCM Kirumba, jijini Mwanza.	Nipashe, 5 Mei 2009, uk. 11.
Makamu wa Rais, Dk Mohamed Shein, Mwanza, 4 Mei 2009.	Afya: Serikali imeahidi kuanza kugharimia matibabu na huduma nyingine za kiafya kwa watu wenye ulemavu wa ngozi nchini (Albino) baada ya Mswada wa Mkataba wa Kimataifa wa Afya, kusainiwa kuwa sheria kamili. Kauli hiyo ilitolewa na Makamu wa Rais, Dk Mohamed Shein wakati akizungumza kwenye maazimisho ya siku ya albino, yaliyofanyika katika uwanja wa CCM Kirumba jijini Mwanaza.	Sitta Tumma, Tanzania Daima, 6 Mei 2009, uk. 5.
Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, John Chiligati, Singida, 4 Mei 2009.	Ardhi (Wataalamu wa ardhi): Halmashauri za wilaya na manispaa mkoani Singida zimeagizwa kuajiri wataalamu wa kutosha katika Idara ya Ardhi ili kukabiliana na changamoto zinazoikabili. Agizo hilo lilitolewa na Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, John Chiligati wakati wa ufunguzi wa semina ya uzinduzi wa mradi wa upimaji na utoaji hati za kumiliki za kimila kwa wananchi iliyofanyika katika Ukumbi wa Kanisa Katoliki mjini Singida.	Elisante John, Nipashe, 6 Mei 2009, uk. 11.
Mbunge wa Jimbo la Maswa, John Shibuda, Mwanza.	Kilimo: Serikali imesema kuwa itanunua pamba yote ambayo haikununuliwa kwa wakulima kwa kipindi cha mwaka 2007/2008 kutokana na mtikisiko wa uchumi wa dunia. Kauli hiyo ilitolewa na Mbunge wa Jimbo la Maswa, John Shibuda katika kikao cha Baraza la Madiwani na Mbunge kilichofanyika jijini Mwanza	Nipashe, 13 Mei 2009, uk. 16

KIONGOZI	AHADI/MAAGIZO	MWANDISHI/GAZETI
Waziri Mkuu, Mizengo Pinda, Sumbawanga, 13 Mei 2009.	Miundombinu (Barabara za vijijini): Serikali imeahidi kuboresha barabara za vijijini ili kuboresha maisha ya wananchi vijijini. Ahadi hiyo ilitolewa na Waziri Mkuu, Mizengo Pinda wakati akihutubia mkutano wa hadhara uliofanyika katika kijiji cha Mamba, wilayani Sumbawanga. Waziri Mkuu alisema kuwa serikali itaendelea kutoa kila aina ya msaada utakaohitajika ili kuboresha miundombinu vijijini. Alisema hatua hii itasaidia kuinua shughuli za kiuchumi katika maeneo ya vijijini ambako asilimia 80 ya Watanzania wanaishi.	Daily News, 14 Mei 2009, uk. 2.
Waziri Mkuu, Mizengo Pinda, Mpanda.	Ulevi: Unywaji wa pombe za kienyeji katika siku za katikati ya wiki umepigwa marufuku isipokuwa Jumamosi na Jumapili ambazo ni siku za mapumziko. Amri hiyo ilitolewa na Waziri Mkuu, Mizengo Pinda wakati akihutubia wananchi wa kata ya Kibaoni, wilayani Mpanda ambako ni mahali alikozaliwa. Waziri Mkuu aliwataka wananchi kuachana na tabia hiyo na badala yake kujishughulisha na shughuli za kimaendeleo.	Daily News, 16 Mei 2009, uk. 1
Waziri wa Elimu na Mafunzo, Profesa Jumanne Maghembe.	Elimu (Malipo ya malimbizo ya walimu): Serikali imesema kwamba madeni ya walimu yatalipwa baada ya zoezi la kuhakiki kukamilika Juni 15, mwaka huu. Kauli hiyo ilitolewa na Waziri wa Elimu na Mafunzo, Profesa Jumanne Maghembe kufuatia kauli ya Chama cha Walimu Tanzania (CWT), kwamba kama siku 15 tangu Ijumaa Mei 15, 2009 zitapita bila kulipa malimbikizo ya madeni yao ambayo yanafikia Sh bilioni 4.4, watagoma na kuvamia Ikulu kushinikiza.	Joseph Mwendaploe, Nipashe, 18 Mei 2009, uk. 1
Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, William Lukuvi, Dar es Salaam.	Usafiri (Msongamano wa magari): Mkuu wa Mkoa wa Dar es salaam, William Lukuvi alisema serikali imejiandaa kupunguza kero ya msongamano wa magari katika jiji la Dar es Salaam. Mkuu wa Mkoa alisema jumla ya shs bilioni 20 zitatumika kupunguza kero hiyo. Mh. Lukuvi aliyasema hayo katika kipindi cha 'Power n' Breakfast' kinachorushwa na redio Clouds FM ya Jijini Dar es Salaam wakati akizungumzia changamoto na vipaumbele vya uongozi wake mara baada ya Rais Jakaya Kikwete kumhamishia Dar es salaam hivi karibuni.	Edward Kinabo, Tanzania Daima, 23 Mei 2009, uk. 5.
Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, John Mwakipesile, 30 May 2009, Mbeya.	Ujenzi: Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, John Mwakipesile ameagiza kuondolewa haraka kutoka katika kamati ya mkoa Mhandisi na msimamizi wa ujenzi wa majengo ya serikali mkoani humo, Bwana Aidan Ngwada kwa tuhuma za kutoa ripoti isiyo sahihi ya miradi ya ujenzi katika ngazi ya mkoa na wilaya. Mwakipesile alitoa amri hiyo kufuatia malalamiko yaliyotolewa na Wakuu wa wilaya za Kyela, Chunya, Mbeya na Mbozi.	Jonas Mwasumbi, Daily News, Juni 1, 2009, uk. 2
Katibu Mkuu, Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, Dk. Charles Nyamrunda, Dar es Salaam.	Ardhi: Serikali imeweka malengo ya kuhakikisha kuwa vijiji vyote nchini vinakuwa na mipango ya matumizi bora ya ardhi ifikapo mwakani. Kauli hiyo ilitolewa na Katibu Mkuu wa Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, Dk. Charles Nyamrunda wakati wa kufunga mradi uliokuwa ukilenga kusaidia migogoro ya ardhi katika jamii za wafugaji hapa nchini.	Pius Rugonzibwa, Daily News, June 1, 2009, uk. 3.
Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, William Lukuvi, Dar es Salaam, 3 Juni 2009.	Fidia kwa wahanga wa mabomu ya Mbagala: Serikali imewahakikishia wahanga wote wa milipuko ya mabomu iliyotokea 29 Aprili 2009 huko Mbagala kuwa itawalipa fidia kulingana na athari walizopata na kwamba hawatahamishwa kupelekwa maeneo mengine. Kauli hiyo ilitolewa na Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, William Lukuvi wakati akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake. Mh. Lukuvi aliyasema hayo mara baada ya kupokea ripoti ya tathmini ya madhara yaliyosababishwa na milipuko ya mabomu hayo katika kambi ya Jeshi la Wanachini wa Watanzania iliyoko Mbagala.	Abdulwakil Saiboko, Daily News, 4 Juni 2009, uk. 1

KIONGOZI	AHADI/MAAGIZO	MWANDISHI/GAZETI
Rais Jakaya Mrisho Kikwete, Dar es salaam.	Kilimo: Serikali imeahidi kuweka mkakati thabiti wa kuendeleza sekta ya kilimo ili kuhakikisha kinaleta tija kubwa kwenye uchumi. Rais aliyasema hayo wakati wa kufunga mkutano wa mashauriano uliowashirikisha wafanyabiashara wa ndani, mawaziri, wakuu wa mikoa, wabunge na wakuu wa wilaya. Mkutano huo uliandaliwa na Baraza la Taifa la Biashara (TNBC) ambalo Rais Kikwete ndiye mwenyekiti wake.	Joseph Mwendapole, Nipashe, 5 Juni 2009, uk. 5.
Rais Jakaya Mrisho Kikwete, Dar es Salaam.	Makazi na uendelezaji miji : Serikali imesema haitawahamisha wakazi wa Kigamboni ili kupisha mradi wa ujenzi wa mji mpya unaotarajiwa kuanza hivi karibuni. Rais aliyasema hayo wakati wa hafla ya ufunguzi wa kivuko kimpya cha Mv Magogoni. Rais alikanusha uvumi kwamba wakazi hao watahamishwa pindi mradi huo utakapoanza.	Nasra Abdallah na Magdalena Paul, Tanzania Daima, 5 Juni 2009, uk. 1.
Rais Jakaya Mrisho Kikwete, Dar es Salaam, 4 Juni 2009.	Miundombinu: Serikali imeahidi kuwa ujenzi wa daraja la Kigamboni jijini Dar es Salaam unatarajiwa kuanza mwakani. Ahadi hiyo ilitolewa na Rais Jakaya Mrisho Kikwete wakati akizindua kivuko kipya cha MV Magogoni. Alisema Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) tayari umeshatangaza tenda ya kumtafuta mkandarasi atakayejenga daraja hilo.	Jiang Alipo na Loyce Joseph, Daily News, 5 Juni 2009, uk. 1.
Waziri Mkuu, Mizengo Pinda, Dodoma, 4 Juni 2009.	Utawala bora: Serikali imeahidi kuongeza kasi ya kupambana na rushwa kubwa ambalo ni tatizo kubwa la kijamii na kiuchumi hapa nichini. Mh. Pinda alitoa ahadi hiyo mjini Dodoma wakati akihutubia wajumbe wa mkutano mkuu wa Baraza la Kikristo Tanzania.	Daily News, 5 Juni 2009, uk.2
Makamu wa Rais, Dk. Ali Mohamed Shein, Tabora, 5 Juni 2009.	Mazingira: Halmashauri zote za wilaya zimeagizwa kuhakikisha kuwa zinakomesha vitendo vyote vya uchomaji moto misitu ambavyo ni chanzo kikuu cha uharibifu wa mazingira. Agizo hilo lilitolewa na Makamu wa Rais, Dk. Ali Mohamed Shein wakati akihutubia katika sherehe za Siku ya Kitaifa ya Mazingira iliyofanyika mkoani Tabora.	The CITIZEN, 6 Juni 2009, uk. 2
Naibu Waziri wa Miundombinu, Hezekiah Chibulunje, Dar es salaam, 5 Juni 2009.	Miundombinu (Fidia kwa upanuzi wa uwanja wa ndege): Serikali imeahidi kuwalipa fidia wakazi wa Kipawa, jijini Dar es Salaam kutokana na nyumba zao kutakiwa kubomolewa ili kupisha upanuzi wa Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere. Ahadi hiyo ilitolewa na Naibu Waziri wa Miundombinu, Hezekiah Chibulunje muda mfupi baada ya kufungua mradi wa upanuzi wa uwanja huo. Alisema malipo hayo yatafanyika mwaka ujao wa fedha (2009/10)	Richard Makore, Nipashe, 6 Juni 2009, uk. 3.
Kamanda wa Polisi wa Kanda Maalum ya Dar es Salaam, Suleiman Kova, Dar es Salaam, 5 Juni 2009.	Ulinzi na usalama: Kamanda wa Polisi wa Kanda Maalum ya Dar es Salaam, Suleiman Kova, amesema vikosi vyake vimejiandaa kupunguza vitendo vya uhalifu jijini Dar es salaam kutoka asilimia 50 ya sasa hadi kufikia robo ifikapo mwakani. Kamanda Kova aliyasema hayo wakati wa sherehe ya kuwakabidhi zawadi na vyeti askari waliofanya vizuri katika kipindi cha mwaka mmoja uliopita.	Romana Mallya, Nipashe, 6 Juni 2009, uk. 3.
Mkuu wa Mkoa wa Dar es salaam, Wlliam Lukuvi, Dar es Salaam.	Usafirishaji (Ajira za madereva wa daladala): Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, William Lukuvi ameagiza kuanza kutekelezwa mara moja kwa makubaliano baina ya vyama vya wafanyakazi wa daladala na wamiliki wa magari hayo ya mwaka 2004 kuhusu ajira. Makubaliano hayo yako katika mkataba ambao uliidhinishwa na kusainiwa na Mahakama Kuu divisheni ya kazi	Editha Majura, Kulikoni, 10 Juni 2009, uk. 3.

KIONGOZI	AHADI/MAAGIZO	MWANDISHI/GAZETI
Kaimu Mkurugenzi, Dr. Mshindo Msolla, Wizara ya Kilimo, Usalama wa Chakula na Ushirika, Mbeya.	Kilimo (Pembejeo): Serikali inatarajia, katika mwaka wa fedha ujao, kuongeza idadi ya mikoa inayopata pembejeo za ruzuku kupitia mfumo wa kipande (voucher system) ili kuwawezesha wakulima wengi kufaidika na mpango huo. Tamko hilo lilitolewa na Kaimu Mkurugenzi wa Pembejeo za kilimo katika Wizara ya Kilimo, Usalama wa Chakula na Ushirika. Kwa sasa mfumo huo tayari unafanya kazi katika mikoa 16 ikiwemo mikoa ya Iringa, Mbeya, Ruvuma, Rukwa, Kigoma, Arusha na Kilimanjaro. Kwa mujibu wa Dr. Msolla, mikoa mipya itakayoingia katika mpango huo ni pamoja na Dodoma, Tanga, Pwani, Lindi, Mtwara, Shinyanga, Tabora na Mara.	Jonas Mwasumbi, Daily News, 8 June 2009, uk. 2.
Waziri Mkuu, Mizengo Pinda, Dar es salaam, 8 Juni 2009.	Nishati: Serikali imeahidi kuwa nchi haitaingia gizani kutokana na matatizo ya umeme kwa kuwa kuna maandalizi ya kutosha katika kukabiliana na hali hiyo. Mh. Pinda alitoa ahadi hiyo mara baada ya kufungua mkutano wa Baraza la Biashara la Afrika Mashsriki (EABC).	Richard makore, Nipashe, 9 Juni 2009, uk. 3.
Waziri Mkuu, Mizengo Pinda, Dodoma.	Uraia (Vitambulisho vya uraia): Serikali imeahidi kuwa inafanya kila jitihada kuhakikisha kuwa vitambulisho vipya vya uraia vinakuwa tayari kabla ya uchaguzi mkuu ujao wa 2010. Waziri Mkuu aliyasema hayo akiwa Bungeni Dodoma wakati akijibu swali la Mh. Mohamed Mnyaa (Mkanyageni-CUF).	The CITIZEN, 12 Juni 2009, uk. 4.
Waziri wa Fedha na Uchumi, Mustafa Mkulo, Dodoma, 11 juni 2009.	Elimu: Serikali imeahidi kujenga nyumba za walimu ili kuwavutia walimu kufanya kazi katika maeneo ya vijijini. Waziri aliyasema hayo wakati akiwasilisha bungeni bajeti ya mwaka huu wa fedha wa 2009/10. Alisema mradi huo utaanzia vijijini ambako walimu wengi hawataki kwenda kutokana na hali duni ya nyumba za walimu.	Beatusi Kagashe, The CITIZEN, 12 Juni 2009, uk. 12.
Waziri wa Maji na Umwagiliaji, Prof. Mark Mwandosya, Dodoma, 12 Juni 2009.	Maji: Serikali imeahidi kuwa tatizo la maji katika sehemu nyingi za jiji litakuwa limekwisha hivi karibuni kufuatia kukamilika kwa mradi wa ujenzi wa bwawa la Kidunda. Ahadi hiyo ilitolewa na Waziri wa Maji na Umwagiliaji, Prof. Mark Mwandosya wakati akijibu maswali ya wabunge Victor Mwambalaswa wa jimbo la Lupa na Zito Kabwe wa jimbo la Kigoma Kaskazini.	The CITIZEN, 13 Juni 2009, uk. 6.
Waziri wa nchi katika Ofisi ya waziri Mkuu (Sera, uratibu na masuala ya Bunge), Philip Marmo, Dodoma, 15 Juni 2009.	Ustawi wa jamii (Fidia kwa wahanga wa mabomu): Serikali imeahidi kuwa itashirikiana na wadau mbali mbali kuhakikisha kuwa hali ya maisha ya wahanga wa mabomu yaliyolipuka hivi karibuni katika kambi ya jeshi huko Mbagala inarejea katika hali ya kawaida. Ahadi hiyo ilitolewa na Waziri wa nchi katika Ofisi ya Waziri Mkuu anayeshughulikia sera, uratibu na masuala ya bunge, Philip Marmo mjini Dodoma wakati akijibu swali la Mbunge wa viti maalum kwa tiketi ya CUF, Ania Chaurembo aliyetaka kujua ni kwa nini kitengo cha maafa kilichopo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu hakikuchukua hatua za haraka kuwasaidia waathirika wa mabomu ya Mbagala.	Daily News, 16 Juni 2009, uk. 2
Naibu Waziri wa Wizara ya Nishati na Madini, Kighoma Malima, Dodoma, 17 Juni 2009.	Nishati: Serikali imetenga bilioni 3/- kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha kusambazia umeme cha Mabuki, katika wilaya ya Kwimba mkoani Mwanza. Kauli hiyo ilitolewa na Naibu Waziri wa Wizara ya Nishati na Madini, Kighoma Malima wakati akijibu swali la mbunge wa Kwimba, Bujiku Sakila.	Benjamin Sawe, Kulikoni, 18 Juni 2009, uk 4.

KIONGOZI	AHADI/MAAGIZO	MWANDISHI/GAZETI
Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, Margaret Sitta, Dar es Salaam, 22 Juni 2009.	Haki za watoto: Serikali imesema ina mipango ya kuanzisha kituo cha kulinda na kutetea haki za watoto nchini. Kauli hiyo ilitolewa na Waziri wa Maendeleo, Jinsia na Watoto, Margaret Sitta wakati akifungua warsha ya kutafuta maoni kutoka kwa wadau juu ya uhalali na namna ya kuanzisha kituo cha kutetea haki za watoto.	Mary Gwera, Daily News, 23 Juni 2009, uk 3
Waziri Mkuu, Mizengo Pinda, Dodoma, 22 Juni 2009.	Demokrasia (Mfumo wa uchaguzi): Serikali imeahidi kufanya marekebisho ya mfumo wa uchaguzi kama sehemu ya juhudi zake za kufanya uchaguzi kuwa huru na wa haki. Sheria zitakazofanyiwa mabadiliko makubwa ni pamoja na Sheria ya Uchaguzi namba 1 ya mwaka 1985 na Sheria ya Serikali za Mitaa (Uchaguzi) namba 4 ya mwaka1979. Ahadi hiyo ilitolewa na waziri Mkuu, Mizengo Pinda wakati akiwasilisha makadirio ya bajeti ya ofisi yake katika mwaka wa fedha 2009/10.	Damas Kanyabwoya, the CITIZEN, 23 Juni 2009, uk. 1.
Naibu Waziri wa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, Dk. Aisha Kigoda, Dodoma 22 Juni 2009.	Afya: Serikali imesema kuwa imeweka mikakati madhubuti ya kukomesha ugonjwa wa malaria nchini. Moja ya mikakati hiyo ni kampeni ya kusambaza vyandarua milioni 7.2 nchi nzima kwa watoto walio chini ya umri wa miaka mitano pamoja na kutoa vyandarua viwili bure kwa kila kaya Tanzania bara. Kauli hiyo ilitolewa na Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, Dk. Aisha Kigoda wakati akijibu swali la Mbunge wa Viti Maalum, Maria Hewa aliyetaka serikali isambaze vyandarua vyenye dawa bure kwa wananchi.	The Citizen, 23 Juni 2009, uk. 4.
Naibu Waziri wa Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana, Dk. Makongoro Mahanga, Dodoma.	Mfuko wa Taifa wa Uwezeshaji (Mabilioni ya JK): Serikali imeahidi kuwa awamu ya pili ya Mfuko wa Taifa wa Uwezeshaji utatoa fedha zake kwa wananchi kwa kupitia Taasisi za fedha zenye matawi yake vijijini kama vile vyama vya kuweka na kukopa ili kuwawezesha Watanzania wengi kufaidika na mfuko huo. Ahadi hiyo ilitolewa na Naibu Waziri wa Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana, Dk. Makongoro Mahanga wakati akijibu swali la nyongeza kutoka kwa Mohamed Misanga, Mbunge wa Singida Kusini. Mh. Misanga alisema kuwa fedha za Mfuko wa taifa wa Uwezeshaji ambazo zimekuwa zikitolewa kupitia benki za CRDB na NMB zimekuwa zikiishia makao makuu ya wilaya na kwa sehemu kubwa waliokuwa wakinufaika nazo ni matajiri wa mijini jambo ambalo ni kinyume kabisa na malengo ya kuanzishwa kwa mfuko huo.	Daily News, 24 Juni 2009, uk. 3.
Naibu Waziri katika Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI), Aggrey Mwanri, Dodoma, 23 Juni 2009.	Afya: Serikali imeahidi kuwa katika mwaka wa fedha ujao itaweka vivutio maalumu kwa waganga wanaofanya kazi katika maeneo ya vijijini. Hatua hiyo imechukuliwa ili kuwavutia waganga na wahudumu wa afya kwenda kufanya kazi katika maeneo ya vijijini ambako hakuna mazingira mazuri ya kuishi na kufanyia kazi. Ahadi hiyo ilitolewa na Naibu waziri katika Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI), Aggrey Mwanri wakati akiwa bungeni Dodoma. Alisema serikali itahakikisha kuwa kuna mgawanyo sawa wa waganga na wahudumu wa afya katika maeneo yote nchini.	Daily News, 24 Juni 2009, uk. 2.
Rais Jakaya Mrisho Kikwete, Tanga, 27 Julai 2009.	Uhaba wa chakula: Wakuu wa Mikoa ambao maeneo yao yanakabiliwa na upungufu wa chakula wameagizwa kufanya tathmini ya hali ya chakula katika maeneo hayo na kutoa taarifa ya mahitaji yao ya chakula ili serikali iweze kutoa msaada wa chakula kwa wakati. Agizo hilo lilitolewa na Rais Jakaya Mrisho Kikwete wilayani Kilindi, mkoa wa Tanga wakati wa ziara ya kukagua miradi mbali mbali ya maendeeleo katika mkoa huo. Rais alisema nchi inacho chakula cha kutosha na kwamba hakuna mtu atakayekufa kwa njaa.	The CITIZEN, 28 Juni 2009, uk. 3

Huu ni mwaka wa nne wa serikali ya awamu ya nne ambayo kauli mbiu yake imekuwa ni ***"Maisha bora kwa kila Mtanzania".*** Ahadi hii ilitolewa na serikali kwa Watanzania wakati ilipoingia madarakani mwaka 2005. Kama ilivyoainishwa katika Dira ya Maendeleo ya Tanzania, 2025 na MKUKUTA, moja ya malengo ya serikali ya awamu ya nne ni kuboresha na kuimarisha utawala bora ili kuleta maendeleo endelevu. Utawala bora una misingi yake, baadhi ya misingi hiyo ni pamoja na utawala wa sheria, uwajibikaji, uwazi, kuheshimu haki za binadamu, demokrasia, kupiga vita rushwa na ufisadi na ushirikishwaji wa wananchi katika masuala yanayowahusu.

Katika jamii yoyote ile ya kidomokrasia, matendo na kauli za viongozi wa serikali vinapaswa kufuatiliwa na wananchi ili kuhakikisha kuwa viongozi au serikali husika inawajibika kikamilifu kwa wananchi ambao ndiyo walioiweka madarakani. Kupitia vyombo vya habari, mikutano na ilani za vyama, serikali imekuwa ikitoa ahadi mbalimbali kwa wananchi na maagizo kwa watendaji wake yenye lengo la kuboresha utendaji wa serikali katika kuwahudumia wananchi. Mwananchi unapaswa kujiuliza, je serikali inatimiza ahadi zake?, kama haitimizi, ni kwa nini? Na kama inatimiza, ni kwa kiasi gani?. Katika ufuatiliaji huu, sifa zinapaswa kutolewa pale inapostahili na maelezo zaidi kudaiwa pale ambapo serikali inashindwa kutekeleza ahadi zake ipasavyo.

Wananchi wanapaswa kuwa na taarifa za kutosha kuhusu ahadi za serikali yao ili waweze kufutilia kikamilifu utekelezaji wake. Hata hivyo wananchi wengi hawajui kuwa hii ni haki yao ya msingi na hawana taarifa juu ya ahadi zinazotolewa na serikali, na hivyo kufanya kazi yao ya kufuatilia kuwa ngumu.

Hali hii imesababisha ahadi nyingi kutotekelezwa. Kuwaelimisha wananchi juu ya haki na wajibu wao pamoja na kuwapa taarifa mbalimbali kuhusu maendeleo yao kutawasaidia sana kufuatilia utendaji wa serikali yao na hivyo kuifanya iwajibike ipasavyo .

HakiElimu inawezesha wananchi kuleta mabadiliko katika elimu na demokrasia

SLP 79401 • Dar es Salaam • Tanzania
Simu: (255 22) 2151852/3 • Faksi: (255 22) 2152449
info@hakielimu.org • www.hakielimu.org